## 3.2 KISWAHILI (102)

### 3.2.1 Utangulizi

Utendaji wa wanafunzi katika somo la Kiswahili unaelekea kuwa hafifu. Hili linadhihirika kwa matokeo ya mtihani wa Kiswahili, hasa ya karatasi ya pili na ya tatu, ambayo yamekuwa yakiyumba mwaka baada ya mwingine tangu kuanzishwa kwa mtaala mpya.Watahini wamekuwa wakishuhudia kushuka kwa viwango vya majibu yanayotolewa na watahiniwa. Kadhalika, kumekuwa na kushuka na kupanda kwa asilimia ya watahiniwa wanaotuzwa gredi za juu. Uchanganuzi huu unanuiwa kutathmini utendaji wa watahiniwa katika karatasi mahususi, na katika somo la Kiswahili kwa jumla. Jedwali lifuatalo linaonyesha matokeo ya mtihani wa somo la Kiswahili katika kipindi cha miaka saba (2012 hadi 2018 ).

**Jedwali 10**: ***Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili (2012 – 2018)***

| Mwaka | Karatasi | Watahiniwa | Upeo | Alama ya Wastani | Alama Tenganishi |
|---|---|---|---|---|---|
| **2012** | **1** | | **40** | 10.43 | 3.63 |
| | **2** | | **80** | 29.06 | 10.77 |
| | **3** | 433,886 | **80** | 32.14 | 15.15 |
| | **Jumla** | | **200** | 71.62 | 25.71 |
| **2013** | **1** | 445,555 | **40** | 18.46 | 5.44 |
| | **2** | | **80** | 29.92 | 12.68 |
| | **3** | | **80** | 34.82 | 14.92 |
| | **Jumla** | | **200** | 83.19 | 29.77 |
| **2014** | **1** | 482,122 | **40** | 20.17 | 5.26 |
| | **2** | | **80** | 32.27 | 12.60 |
| | **3** | | **80** | 42.93 | 15.81 |
| | **Jumla** | | **200** | 95.36 | 29.88 |
| **2015** | **1** | 5211,59 | **40** | 20.86 | 5.19 |
| | **2** | | **80** | 36.12 | 13.50 |
| | **3** | | **80** | 38.80 | 15.38 |
| | **Jumla** | | **200** | 95.76 | 31.02 |
| **2016** | **1** | 571,176 | **40** | 18.23 | 5.53 |
| | **2** | | **80** | 34.11 | 13.83 |
| | **3** | | **80** | 25.67 | 12.87 |
| | **Jumla** | | **200** | 77.97 | 29.07 |
| **2017** | **1** | 610,392 | **40** | 18.84 | 5.23 |
| | **2** | | **80** | 25.45 | 11.79 |
| | **3** | | **80** | 25.15 | 13.42 |
| | **Jumla** | | **200** | 69.43 | 27.49 |
| **2018** | **1** | 659,465 | **40** | 16.98 | 4.82 |
| | **2** | | **80** | 27.22 | 10.88 |
| | **4** | | **80** | 22.20 | 11.95 |
| | **Jumla** | | **200** | 66.40 | 24.76 |

https://kcserevision.com

Kutokana na jedwali hili, pamoja na takwimu na ripoti nyingine za uchanganuzi wa karatasi za mitihani ya Kiswahili ya mwaka huu, imedhihirika kwamba kwa jumla:

i) Utendaji wa wanafunzi katika utungaji umedhoofika. Haya yanadhihirishwa na kushuka kwa alama wastani ya karatasi ya kwanza (102/1) kutoka **18.84** ya mwaka 2017 hadi **16.98** mwaka huu. Alama ya juu zaidi iliyotuzwa ni **38/40**. Ni mwanafunzi **mmoja** tu ambaye alipata alama hii. Hali kadhalika, wanafunzi **4,221** ndio ambao walipata asilimia sabini **(70%- 28/40)** katika karatasi hii. Hii ni asilimia ndogo mno ya watahiniwa **659,465** ambao walifanya mtihani huu.

ii) Aidha karatasi ya kwanza bado haijawatenga vyema wanafunzi bora na wale hafifu.Hili linadhihirishwa na alama tenganisho **(4.82)** ambayo iko chini sana ikilinganishwa na alama ya tenganisho ya kikaida **(15.00).** Hali hii inaweza kusababishwa na watahini kuongozwa na kutawaliwa na mtazamo nafsi wakati wa kuzitathmini insha za watahiniwa na kuishia kuwaweka katika viwango sawa au vinavyokaribiana.

iii) Alama ya wastani ya karatasi ya pili (102/2) imepanda kidogo kutoka **25.43** mwaka **2017** hadi **27.22** mwaka huu. Alama ya juu zaidi iliyotuzwa ni **70/80.** Ni mwanafunzi **mmoja** tu ambaye alipata alama hii. Hali kadhalika, ni wanafunzi **1,007** tu ambao walipata asilimia sabini **(70%- 56/80)** katika karatasi hii. Hii ni asilimia ndogo mno ya watahiniwa **659,465** ambao walifanya mtihani huu. Hata hivyo, imebainika kwamba karatasi hii iliweza kuwatenga vyema wanafunzi bora na wale hafifu. Alama tenganisho ilikuwa **10.88,** japo alama hii imeshuka kutoka **11.79** ya mwaka 2017.

iv) Utendaji wa watahiniwa katika karatasi ya pili (102/2) unaendelea kudorora. Ruwaza za matokeo zaonyesha kuwa matokeo ya karatasi hii yamezidi kuyumba tangu mwaka wa 2009. Alama ya wastani ilishuka kwa takriban alama **kumi (10)** mwaka 2010, ikapanda kwa takriban kiwango hichohicho mwaka 2011, na baadaye kushuka kwa alama **kumi na nne nukta tatu sufuri (14.30)** mwaka 2012. Mwaka 2013 ilipanda kwa kiasi kidogo mno, mwaka 2014 kwa **2.35**, na mwaka 2015 kwa takriban alama 4. Mwaka 2016 alama ilishuka kwa takriban alama **mbili.** Mwaka 2017 alama hii ilishuka kwa zaidi ya alama **8.** Hata hivyo, mwaka huu alama imepanda kwa takriban alama **2**.

https://kcserevision.com

v) Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya mwaka wa 2018 yameshuka kwa takriban alama **3** kutoka alama wastani **25.65** hadi **22.20** mwaka huu. Alama ya juu zaidi iliyotuzwa ni **72/80.** Ni wanafunzi **wawili** tu waliopata alama hii. Hali kadhalika, ni wanafunzi **540** tu ambao walipata asilimia sabini **(70%- 56/80)** katika karatasi hii. Hii ni asilimia ndogo mno ya watahiniwa **659,465** ambao walifanya mtihani huu.

vi) Alama wastani ya somo la Kisahili kwa jumla imeshuka kwa takriban alama **3** kutoka **69.43** mwaka 2017 hadi **66.40** ya mwaka huu.

vii) Asilimia ya watahiniwa wanaopata gredi A na A- ni ndogo mno.

viii) Alama wastani ya somo hili bado haijafikia kiwango cha kuridhisha.

## 3.2 Uchanganuzi wa karatasi mahususi

### 3.2.1 Kiswahili Insha (102/1)

***Jedwali 11: Matokeo ya Karatasi ya kwanza ya miaka 2012 – 2018***

| Mwaka | **2012** | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 10.43 | 18.46 | 20.17 | 20.86 | 18.23 | 18.84 | 16.98 |
| Alama ya Tenganisho | 3.63 | 5.44 | 5.26 | 5.19 | 5.53 | 5.23 | 4.82 |

Jedwali hili linaonyesha kwamba kwa kipindi cha miaka minne (2015 - 2018), utendaji wa watahiniwa katika karatasi hii umekuwa ukiyumba. Tathmini ya kazi halisi za watahiniwa imebainisha kwamba asilimia kubwa ya watahiniwa haimudu kujieleza kwa lugha iliyokomaa. Ni wazi kwamba idadi kubwa ya watahiniwa haikuweza kukuza mada inavyostahili. Aidha, asilimia kubwa ya watahiniwa walipata chini ya nusu ya alama zilizotengewa karatasi hii. Wengi walipata alama **16/40**, au chini. Tathmini ya kazi za watahiniwa pia imeonyesha kwamba watahiniwa wengi hawamudu tungo za kiuamilifu. Wengi wanazingatia muundo wa tungo hizi bila kushughulikia maudhui ya swali kikamilifu. Hii ni ishara kwamba wanafunzi wengi hawana mazoea ya kusoma kwa kina. Hata hivyo, imebainika kwamba idadi ya watahiniwa wanaoteua swali linalohusiana na methali imeongezeka kiasi, japo bado i chini. Hili linadokeza kwamba ule mtazamo wa kijadi kuwa insha zinazohusu methali huwa ngumu umeanza kubadilika.

Tazama uchanganuzi wa swali la kwanza ambalo ndilo lililokuwa la lazima.

**1. Lazima**

**Wewe ni katibu wa chama cha Walinda Mazingira Wasio na Mipaka shuleni mwenu. Andika kumbukumbu za mkutano uliofanyika kujadili suala la uharibifu wa mazingira katika eneo lenu.**

Swali hili lilimhitaji mtahiniwa kuandika kumbukumbu za mkutano wa Chama cha Walinda Mazingira wasio na Mipaka kuhusu uharibifu wa mazingira. Watahiniwa wengi walimudu kuzingatia muundo wa nje wa utungo wa aina hii.

https://kcserevision.com

Hata hivyo, tungo za watahiniwa zilidhihirisha kwamba wengi wamekosa ubunifu. Wengi hawakuweza kujadili hoja zilizotarajiwa; wakashindwa kukuza mada kikamilifu. Ni muhimu kukumbuka kuwa watahiniwa walikosa ubunifu hata katika maswali yale mengine.

Imebainika kwamba wanafunzi wengi hawasomi kwa mapana, hivyo hawadiriki kushughulikia masuala mtambuko ipasavyo katika tungo zao.

### 3.2.2 Ushauri kwa walimu

Walimu wawatayarishe wanafunzi wao katika maeneo yote bila ubaguzi, kulingana na mahitaji ya silabasi ya Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya(KICD).

**Mapendekezo**

i) Walimu wazidi kuwapa wanafunzi mazoezi zaidi katika uandishi wa kiuamilifu.

ii) Walimu watumie silabasi ya K.I.C.D ili kuelekeza ufundishaji wao. Mwongozo unaotolewa na KNEC kuhusu mada na stadi zinazotahiniwa, pamoja na vitabu vya Fasihi vinavyotahiniwa, utumiwe kujalizana na silabasi ya KICD.

iii) Wanafunzi wahimizwe kusoma kwa mapana, na kwa kina (magazeti, majarida, kazi za kifasihi, na vitabu katika nyanja anuwai) ili kujifahamisha kuhusu matukio ya kila siku katika jamii na mazingira yao, kitaifa na pia kimataifa. Hili litapalilia ubunifu wao na kuwawezesha kumudu maswali yanayohusu masuala mtambuko iwapo yatatahiniwa. Haitoshi kujifunga katika masuala yaliyo vitabuni pekee.

iv) Wanafunzi waongozwe na kuelekezwa kuhusu mikakati ifaayo ya kufasiri maswali. kwa uangalifu mkubwa huku wakizingatia maneno muhimu.

### 3.2.2 Kiswahili Lugha (102/2)

**Jedwali 12**: *Matokeo ya Karatasi ya pili (102/2) ya miaka 2012 hadi 2018*

| Mwaka | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Alama ya Wastani** | 29.06 | 29.92 | 32.27 | 36.12 | 34.11 | 25.45 | 27.22 |
| **Alama ya Tenganisho** | 10.77 | 12.68 | 12.60 | 13.50 | 13.83 | 13.42 | 10.88 |

Matokeo ya karatasi ya 102/2 yamepanda kiasi kutoka **25.45** mwaka 2017 hadi **27.22** mwaka huu. Swali la kwanza, la tatu na la nne ndiyo yaliyowatatiza watahiniwa zaidi, Asilimia kubwa ya watahiniwa hawakumudu kujibu maswali yaliyowahitaji kutumia ujuzi wao kupata majibu. Haya ni maswali yanayolenga kukuza stadi za kiwango cha juu cha utambuzi.

Tutachanganua swali la tatu.

**3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

(a) Andika sauti zenye sifa zifuatazo: (alama 2)

(i) kipasuo ghuna cha midomoni

(ii) irabu ya kati, chini

https://kcserevision.com

(iii) kikwamizo sighuna cha kaakaa gumu

(iv) nazali ya ufizi

(b) Bainisha silabi zilizowekewa shadda katika maneno yafuatayo: (alama 1)

(i) miambakofi

(ii) yatazoleka

(c) Andika neno lenye muundo ufuatao: (alama 2)

(i) kiambishi ngeli, wakati uliopita, mzizi, kauli tendwa, kauli tenda (kiishio)

(iii) kiambishi cha wingi, mzizi

(d) Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo. (alama 4)

(i) Uaminifu wa mtu humfanya aheshimiwe.
(Badilisha nomino iliyopigiwa mstari kuwa kivumishi.)

(ii) Shama, Tegea na Koru ndio walioibuka washindi.
(Tumia kiwakilishi nafsi badala ya maneno yaliyopigiwa mstari.)

(iii) Mchuuzi alinunua mboga zilizofungwa pamoja.
(Tumia nomino ya jamii badala ya maneno yaliyopigiwa mstari.)

(iv) Seluwa ni mtiifu. Maria ni mtiifu pia.
(Unganisha kuwa sentensi moja yenye kihusishi cha kulinganisha.)

(e) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? (alama 1)

(i) ugwe ..........................................................................................................
(ii) limau ..........................................................................................................

(f) Unganisha sentensi zifuatazo kuunda sentensi ya masharti. (alama 2)
Moto ulidhibitiwa. Kulikuwa na vifaa vya kutosha.

(g) Andika sentensi ifuatayo katika wingi. (alama 1)

Nahodha alilikwepa jabali hilo, chombo kikafika ufuoni salama.

(h) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama 2)
nomino, kishazi kitegemezi, kitenzi, nomino, kivumishi, kielezi

(i) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali ya mazoea. (alama 1)
Barabara nyingi zimesakafiwa.

(j) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kuanza kwa neno: Wanafunzi. (alama 2)
Wageni wamefika. Wanafunzi wamefurahi.

https://kcserevision.com

(k) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa.

Nguo ambazo zinauzwa kwenye duka hilo zinavutia. (alama 1)

(l) Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo. (alama 4)

(i) Muutu aliwalea watoto wa Maki. (Anza kwa: Watoto wa Maki.)

(ii) Maji yalijaa. Maji yalimwagika. (Unganisha kuunda sentensi changamano.)

(m) Tumia kielezi cha kiasi badala ya kile kilichopigiwa mstari. ( alama 1)
Sewe alituelezea jambo hilo <u>kinaganaga.</u>

(n) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Viongozi wengi walikuwa waadilifu mno kabla ya Uchaguzi Mkuu.

(o) Changanua sentensi zifuatazo kwa kielelezo cha mstari.

(i) Hili lake lilikuwa limeiva lakini hatukujua. (alama 2)

(ii) Mkufu wa Umu unapendeza mno. (alama 1)

(p) Andika maana **mbili** zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo.
Medi anasema atawarithisha nyumba yake. (alama 2)

(q) Akifisha sentensi ifuatayo.
jihadhari akasema kulei uamuzi wako unaweza kukuathiri vibaya. (alama 2)

(r) Kanusha sentensi ifuatayo.
Mkulima anahitaji magunia haya. (alama 1)

(s) (i) Karimu ni kwa choyo .......................... ni kwa kukashifu na .................... ni kwa tele. (alama 2)

(ii) Maarufu ni kwa mashuhuri, ukoo ni kwa ............................... ilhali faida ni kwa .......................... (alama 2)

(t) Tunga sentensi **moja** kubainisha maana **mbili** za neno: kata. (alama 2)

Maswali katika sehemu hii yalilenga mada mbalimbali za kisarufi kama zilivyopendekezwa na silabasi.Maswali yalimhitaji mtahiniwa kutumia ujuzi wake wa dhana za kisarufi kujibu maswali aliyopewa. Imebainika kwamba utendaji wa wanafunzi katika dhana za kimsingi za lugha kama vile kuandika katika umoja, miundo ya maneno, kuandika visawe na uchanganuzi wa sentensi za kimsingi unaendelea kuwa hafifu. Wengine walishindwa kujibu maswali ya kimsingi ya matamshi bora. Kadhalika, watahiniwa wengi mno walipoteza alama katika maswali maalum, hata ya ufahamu na ufupisho, kutokana na makosa ya sarufi na hijai. Wengine hawakumudu kuandika ufupisho ipasavyo; walinakili yale yaliyokuwa katika kifungu.

3.

https://kcserevision.com

(a)

(i) /b/, /m/
(ii) /a/
(iii) /sh/
(iv) /n/

4 x ½ = 2

(b)

(i) Miambakofi
(ii) Yatazoleka

2 x ½ = 1

(c)

(i) ki – li – nunu – liw – a
wa – li – tembe – lew – a
zi – li – jeng – ew – a

Alama 1/0

(ii) Mi-kate – {mi} wingi
{kate} – mzizi
Vi-ti {vi} – wingi
{ti} – mzizi
Ny-ufa {ny} – wingi
{ufa} – mzizi

Alama 1/0

(d)

(i) Mtu mwaminifu huheshimiwa.

Alama – 1/0

(ii) Wao ndio walioibuka washindi.

Alama – 1/0

(iii) Mchuuzi alinunua kicha cha mboga.

Alama 1/0

(iv) Seluwa ni mtiifu kama Maria /
Seluwa ni mtiifu kuliko Maria.

Alama 1/0

(e)

(i) Ugwe – U – ZI.

Alama 1/2

(ii) Limau – LI – YA

Alama 1/2

(f)

(i) Vifaa vya kutosha visingalikuwapo moto usingalidhibitiwa.
(ii) Kama vifaa vya kutosha visingekuwepo moto usingedhibitiwa.
(iii) Kama pasingekuwa na vifaa vya kutosha moto haingedhibitiwa.
(iv) Vifaa vya kutosha visingekuwepo moto usingedhibitiwa.

1 x 2 = 2

https://kcserevision.com

(g) Manahodha waliyakwepa majabali hayo vyombo vikafika fuoni salama.

Alama 1/0

(h) Kwa mfano: Wanafunzi waliotia bidii masomoni walipata alama nzuri mno.

| Wanafunzi | waliotia bidii masomoni | walipata | alama | nzuri | mno. |
|---|---|---|---|---|---|
| Nomino | kishazi kitegemezi | kitenzi | Nomino | kivumishi | kielezi |

Alama 2/0

(i) Barabara nyingi zitakuwa zikisakafiwa.
au
Barabara nyingi zitakuwa zinasakafiwa.

Alama 1/0

(j) Wanafunzi wamefurahia kufika kwa wageni.
Au
Wanafunzi wamefurahi wageni walipofika.
Au
Wanafunzi wamefurahi baada ya wageni kufika.

Alama 2/0

(k) Maguo ambayo yanauzwa kwenye majiduka hayo yanavutia.

Alama 1/0

(l)

(i) Watoto wa Maki walilelewa na Muutu.

Alama 2/0

(ii) Maji yalipojaa yalimwagika.
Au
Maji yalijaa yakamwagika.
Au
Maji yaliyojaa yalimwagika.
Au
Baada ya maji kujaa yalimwagika.

Alama 2/0

(m) Sewe alituelezea jambo hilo tena.
Au
Sewe alituelezea jambo hilo mara mbili/mara kwa mara.

Alama 1/0

(n) viongozi wengi – kirai nomino
walikuwa waadilifu mno – Kirai tenzi
waadilifu mno – kirai vumishi
kabla ya uchaguzi mkuu – kirai husishi
uchaguzi mkuu – kirai nomino.

4 x ½ = 2

(o)

(i) KN (W + V) +KT (TS + T) + U + KN (Ø) + KT (T)

https://kcserevision.com

Alama 2/0

(ii) KN(N+KH)KT(T+E) Au KN( N+W+N) +KT( T+E)

Alama 1/0

(p)

(i) Nyumba ni ya Medi.
(ii) Nyumba ni ya mtu mwingine.
(iii) Medi ndiye atairithisha nyumba.
(iv) Mtu mwingine ndiye atairithisha nyumba.
(v) Nyinyi (nafsi ya pili) ndio mtakaorithishwa.
(vi) Wao (nafsi ya tatu) ndio watakaorithishwa.

2 x 1 = 2

(q) "Jihadhari" akasema Kulei, "uamuzi wako unaweza kukuathiri vibaya."

4 x ½ = 2

(r) Mkulima hahitaji magunia haya.

Alama 1/0

(s)

(i) kusifu – kukashifu
kupongeza – kukashifu
chache / haba/kidogo – tele

2 x 1 = 2

(iii) Nasaba/akraba/mlango/ - ukoo
Natija/tija – faida

2 x 1 = 2

(t) Maana zifuatazo zijitokeze:
(i)Kugawanya/kutenganisha, pengine kwa kisu.
(ii) Ondoa sehemu ya kitu, kwa mfano, kukata ujira/kupunguza kitu.
(iii) Chombo cha kuchotea maji mtunguni.
(iv) Eneo la ardhi/sehemu inayoongozwa na kiongozi fulani k.v. Lokesheni.
(v) Kitambaa au majani yaliyoviringwa kwa ajili ya kuwekwa kichwani kubebea mzigo.

2x1=2

**MAPENDEKEZO**

i) Walimu waendelee kuwapa wanafunzi mazoezi katika vipengele vyote vya kisarufi.

ii) Wanafunzi wasisitiziwe kwamba baadhi ya maswali ni ya stadi za juu kama vile matumizi/ utekelezaji na usanisi. Wasitarajie kila mara kupata maswali ya kuchopoa majibu moja kwa moja kutoka kwenye vifungu au kukariri kutoka kumbukumbu zao.

iii) Wanafunzi wapewe mazoezi ya ufahamu na muhtasari mara kwa mara huku wakihimizwa kuzingatia mtiririko ufaao ili wapate kuzoea kutumia viunganishi kutiririsha hoja katika kujibu maswali ya muhtasari.

iv) Walimu wasisitize vipengele vya kimsingi vya sarufi kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha nne.

https://kcserevision.com

v) Mwelekeo mseto katika ufunzaji uzingatiwe zaidi. Mathalan mwalimu anaweza kutumia Fasihi kufunzia mada tata za sarufi, kama vile aina za sentensi. Hili litachangia katika kulihuisha somo la sarufi na kuwafanya wanafunzi kulichangamkia.

vi) Walimu na wanafunzi watalii maeneo yote ya sajili bila ya kujifunga kwa chache tu ambazo ni za kawaida.

vii)Masuala yote katika silabasi yafundishwe katika upana wayo bila kubagua.

### 3.2.3 Kiswahili Fasihi (102/3)

**Jedwali 13**: ***Matokeo ya Karatasi ya tatu (102/3) ya miaka 2012 hadi 2018***

| Mwaka | **2012** | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 32.14 | 34.82 | 42.93 | 38.80 | 25.67 | 25.15 | 22.20 |
| Alama ya Tenganisho | 15.15 | 14.92 | 15.81 | 15.38 | 12.87 | 13.42 | 11.95 |

Matokeo haya yanaonyesha kuwa utendaji wa watahiniwa katika karatasi hii unaendelea kudorora. Tathmini ya karatasi halisi za watahiniwa ilibainisha kwamba asilimia kubwa ya watahiniwa, hata wale wanaopata alama za juu zaidi katika karatasi hii, haimudu kuwasilisha hoja kwa njia komavu. Kazi za watahiniwa zimepwezwa na makosa mengi ya kisarufi, kimuundo na hijai. Kadhalika, pameibuka mtindo wa kuwasilisha hoja kwa ufupi mno, kiasi cha kuwafanya baadhi ya watahiniwa kupoteza alama. Maswali ya ushairi yanaepukwa na watahiniwa wengi mno. Hata wale wanaodiriki kuyafanya,

wanaambulia alama za chini mno. Imebainika kwamba baadhi ya masuala ya kimsingi ya ushairi hayafunzwi, hivyo yanapotokea katika mtihani watahiniwa wengi hupoteza alama.

Hali kadhalika, karatasi za watahiniwa zimebainisha kwamba changamoto kuu inayoukumba utendaji wa wanafunzi katika Fasihi ni kutosoma vitabu viteule. Ithibati ya haya ni kuchanganya kwa wahusika; mtahiniwa akatumia jina la mhusika wa kitabu kingine kumrejelea wa kitabu anachojibia swali, kutomudu maswali ya muktadha, pamoja na yale ambayo yanamhitaji mwanafunzi kujadili maudhui na dhamira ya kazi husika.

Tutachanganua swali la kwanza kwani ndilo lililokuwa la lazima.

## SEHEMU A : USHAIRI

**1. Lazima**

A. Mazrui: *Chembe Cha Moyo*
*Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Nimeyaandika maneno haya
        Kwa niaba ya:
        Mamilioni wasio malazi
        wabebao vifurushi vilivyo wazi
        wazungukao barabarani bila mavazi
        ...milki yao ya maisha.
https://kcserevision.com
Kwa niaba ya:
Maelfu wanouawa bila haki
wiki baada ya wiki
        leo sumu au spaki
        leo kamba au bunduki
na kwa wale wanosubiri kunyongwa.

Kwa niaba ya:
Vijana walio mitaani
wale mayatima wa maskini
wazungukao mapipani
kila pembe mjini
kuokota sumu kutia tumboni
kujiua bila kujua
ili kupata kuishi.

Kwa niaba ya:
Wakongwe wasiojiweza
walao chakula kilichooza
wachukuao choo wakijipakaza
polepole wakijiangamiza
katika vyumba vyao
baridi na giza
kwa sababu hawana watazama
wala wauguza.

Kwa niaba ya:
Waishi na nyingi hofu
kwa sababu ya madawa tifutifu
yatiwayo vyakulani yakitufanya wafu
bila ya mtu kuona
    kama kwamba sote tu vipofu

Na kwa niaba yetu sote;
    Tuliofungwa vifungoni, duniani
    Tuliosukumwa kingoni, maishani
    Tuliopokonywa maoni, machoni
    Tuliotiliwa sumu, malishoni
    Tuliodidimizwa kinyesini
        ili 'maendeleo'
        yaendelee kwenda njiani
        huku yakitema machicha ya roho zetu.

(a) "Shairi hili linakatisha tamaa." Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano **saba** kutoka kwenye shairi. (alama 7)

(b) Fafanua umuhimu wa aina **mbili** za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 4)

(c) Bainisha vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili. (alama 3)

(i) tasfida

(ii) kinaya

(iii) tashihisi

(d) Eleza kwa kutoa mfano, mbinu **moja** ambayo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika ubeti wa **tano**. (alama 2)

(e) Andika ubeti wa **pili** kwa lugha ya nathari. (alama 2)

(f) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 2)

https://kcserevision.com

Swali hili lilimhitaji mtahiniwa kuchanganua vipengele vya kimsingi vya uchanganuzi wa Ushairi; dhamira, tamathali za usemi, uhuru wa kishairi, nafsineni na kuandika kwa lugha ya nathari.

Uchanganuzi wa majibu ya watahiniwa umedhihirisha viwango vya chini vya utendaji wa wanafunzi katika Ushairi. Asilimia kubwa ya watahiniwa haimudu maswali yanayowahitaji kutumia ujuzi wao wa Ushairi kujibia. Udhaifu huu pia umejitokeza katika majibu yao kwa maswali mengine.

1.

(a) Mtahiniwa abainishe hali duni ya maisha (au matatizo) ambayo nafsineni inaangazia.
Mifano:

(i) Umaskini – Kuzunguka barabarani bila mavazi.
- Vifurushi vitupu ndivyo milki yao. (ubeti 1)

(ii) Ukiukaji wa haki za kibinadamu – watu wengi wanauawa bila haki kila wakati. (ubeti 2)

(iii) Tatizo la uyatima – vijana mayatima wa maskini kuzunguka mitaani. (ubeti 3)

(iv) Vijana wanajidhalilisha kwa kula vyakula duni na hatari (kwa sababu ya uhitaji) bila kujua kwamba wanajiua katika harakati zao za kung'ang'ania kuishi. (ubeti 3)

(v) Wazee wanatelekezwa katika makao ya wazee – hawana walinzi wala wauguzi. (ubeti 4)

(vi) Wazee wanauawa polepole kwa kupewa chakula chenye vijasumu (kilichooza) (ubeti 4).

(vii) Wakongwe wamepoteza urazini – hali yao inasikitisha kwani wanajipakaza hata choo. (ubeti 4)

(viii) Mazingira mabaya/magumu kwenye makao ya wazee yanakatisha tamaa. Wanaishi kwenye vyumba vyenye baridi na giza. (ubeti 4)

(ix) Binadamu wamejawa na dhiki ya kisaikolojia. Wanaishi k.wa hofu kwa sababu ya vijasumu vyenye kutiwa kwenye chakula na kuhatarisha maisha yao. (ubeti 5)

(x) Mapuuza – watu wanakula vyakula vyenye sumu/dawa bila kuwazia hatari yake. (ubeti 5)

(xi) Watu wanadhulumiwa; wanafungwa na kukatishwa tamaa (tuliosukumwa kingoni maishani) na kadhalilishwa (tuliodidimiziwa kinyesini) ili maendeleo yapatikane, huku wao wakiwa katika hatari ya kufa.

https://kcserevision.com

(xii) Watu kulemazwa: wanapokonywa uoni( Ubeti wa 6)

(xiii) Kuwepo kwa viongozi wasiowajibika: wanaendeleza shughul za kimaendeleo ambazo zinahatarisha maisha ya wanyonge

**7x 1 = 7**

**(b)**

(i) **Urudiaji wa silabi/silabi zinazosikika kama sauti moja**. Kwa mfano:
zi – katika: makazi, na mavazi (ubeti 1)
ki– katika: haki, wiki, spaki, bunduki (ubeti 2)
ni – katika: mitaani, maskini mapipani, tumboni (ubeti 3)
za – katika: wasiojiweza, kilichooza, wakijiangamiza (ubeti 4)
fu – katika: hofu, tifutifu, wafu (ubeti 5)
**Umuhimu:** kujenga ridhimu/kulipa shairi muonjo/mdundo wa kimuziki/ kuleta urari wa vina.
**Aina** – alama 1
**Umuhimu** – alama 1

(ii) **Urudiaji wa irabu/ sauti.** Kwa mfano.
'o' – katika: wazungukao, wabebao (ubeti 1)
**Umuhimu:** Kujenga ridhimu/kulipa shairi muonjo/mdundo wa kimuziki/ kuleta urari wa vina.
**Aina** – alama 1
**Umuhimu** – alama 1

(iii) **Urudiaji wa vifungu vya maneno**

Kirai: "Kwa niaba ya" kimerudiwa katika shairi zima (ndicho kinaanzia kila ubeti isipokuwa ubeti wa kwanza).

**Umuhimu**

i) Unasisitiza wazo kuu, kwamba nafsineni haijisemei tu – ni sauti ya wanyonge wanaoteseka.

ii) Kuchimuza/ kutambulisha toni ya shairi- nafsineni inachukizwa na hali ya maisha.

**Aina** – alama 1

**Umuhimu** – alama 1

(iv) **Usambamba** – urudiaji wa miundo sawa ya sentensi/vishazi/virai. Kwa mfano:

(i) Leo sumu au spaki
Leo kamba au bunduki (ubeti 2)

(ii) Tuliofungwa vifungoni, duniani
Tuliosukumwa kingoni, maishani

**Umuhimu**

i) Kuonyesha mtazamo wa nafsineni kuhusu masuala anayoibua; anayokashifu.

ii) Kuchimuza toni ya shairi – chuki, masikitiko

**Aina** – alama 1

**Umuhimu** – alama 1

Aina zozote 2 x2 =4

(c)

(i) **Tasfida**

1. **Choo** badala ya mavi. (Ubeti 4)
2. **Kinyesini** badala ya kwenye mavi (Ubeti 6)

https://kcserevision.com

**1 x 1 = 1**

(ii) **Kinaya**

1. Ni kinaya kwamba vijana mitaani wanaokota chakula mapipani ili kuulinda uhai wao lakini vyakula hivi vina vijasumu ambavyo vinawaua polepole bila wao kujua. (ubeti 3)
2. Nchi yaendelea huku ikiwaua watu polepole (Ubeti wa 6).

**1x 1 = 1**

iii) **Tashihisi** – maendeleo yaendelee kwenda njiani huku yakitema machicha ya roho zetu (Ubeti wa 6).

**1 x 1 = 1**

(d) Kufinyanga sarufi/ Kubananga lugha – **nyingi hofu**, badala ya **hofu nyingi**.
Imetumiwa ili kuleta urari wa vina.

**1 x 2 = 2**

**Kutaja**- alama 1, mfano- alama 1

(e) Nimeyaandika (maneno haya) kwa niaba ya (kuwatetea/kuonyesha dhiki za) wengi ambao wanauawa bila sababu (haki/kosa) kila wiki, kwa kutumia sumu, spaki, kamba au bunduki. Nimeandika pia Kwa niaba ya wale wanaosubiri kunyongwa.

**2 x 1**

Wanaouawa bila haki – 1

Wanaosubiri kunyongwa – 1

(f) Nafsineni ni mtetezi wa haki / mtu ambaye amechukizwa na hali ya maisha ya wanyonge na kujitolea kulalamika kwa niaba yao. Mfano. Ninaandika kwa niaba ya .....
**Maelezo** – alama 1
**Mfano** – alama 1

**MAPENDEKEZO**

i) Walimu wafundishe vitabu vilivyoteuliwa kwa ukamilifu huku wakizingatia vipengele vifuatavyo vya uchanganuzi wa kazi za kifasihi:

ii) **Dhamira na maudhui**

iii) **Fani** , kama vile:

- Mandhari- Maana na umuhimu wayo
- Ploti- vipengele kama vile mbinu rejeshi, elekezi na sadfa
- Usimulizi- nafsi na wakati katika usimulizi
- Wahusika- Sifa na umuhimu wao katika kuzijenga kazi za kifasihi
- Muundo- urudiaji, usambamba....
- Mtindo, kama vile tamathali za usemi

iv) Wanafunzi wahimizwe kutambua masuala muhimu yanayojitokeza katika hadithi zote katika diwani teule ya hadithi fupi.

https://kcserevision.com

v) Wanafunzi wawekewe misingi bora katika Fasihi Simulizi tangu kidato cha kwanza.

vi) Walimu wawaelekeze wanafunzi wao kutambua na kutumia istilahi muhimu za ushairi ili kuupalilia ukakamavu wao katika kuyajibu maswali ya Ushairi.

vi) Mbinu za kuchanganua Ushairi zifunzwe katika upana na kina kulingana na kiwango hiki.

vii) La muhimu zaidi wakumbushwe kwamba vipengele vya kazi ya kifasihi ni vilevile. Mathalani, taswira na toni huweza kuchanganuliwa katika Ushairi, na vilevile katika tamthilia na tungo za kinathari.

## 3.5 Hitimisho

Kutokana na uchanganuzi wa hapo juu, ni dhahiri kwamba utendaji wa wanafunzi katika somo la Kiswahili unaendelea kushuka; matokeo ya watahiniwa katika somo la Kiswahili bado hayajafikia kiwango cha kuridhisha. Ni watahiniwa wachache mno waliofikia viwango vya juu vya utendaji katika karatasi zote tatu. Asilimia kubwa ya watahiniwa inapata chini ya alama wastani katika karatasi zote.

Inatumainiwa kwamba walimu na wanafunzi watafaidi kwa uchanganuzi uliotolewa kadhalika ni muhimu kuyatilia maanani mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii ili kuimarisha matokeo ya somo hili. Muhimu zaidi, ipo haja ya kuandaa warsha na makongamano ili kufanikisha kujadiliwa kwa mada na stadi ambazo zinaelekea kuwatatiza wanafunzi zaidi.